**MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ROBO YA TATU 2016/2017 ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA NEWALA TAREHE 24/04/2017.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. | Chitwanga R. Ndembo | - Diwani Mtunguru | -Mwenyekiti |
| 2. | Ndg. | Musa M. Chimae | - Mkurugenzi Mtendaji | -Katibu |
| 3. | Mhe. | Swalehe F. Amri | - Diwani Chitekete | -Mjumbe |
| 4. | Mhe. | Salehe M. Kamtwanje | - Diwani Mpwapwa | -Mjumbe |
| 5. | Mhe. | Hashimu B. Namawa | - Diwani M/Mpelepele | -Mjumbe |
| 6. | Mhe. | Mohamed A. Mnyolokoto | - Diwani Muungano | -Mjumbe |
| 7. | Mhe. | Shaibu R. Ngumbe | - Diwani Kitangari | -Mjumbe |
| 8. | Mhe. | Zaituni L. Nawanda | -Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 9. | Mhe. | Saidi Y. Mawangwa | - Diwani Makukwe | -Mjumbe |
| 10. | Mhe. | Menas M. Likuku | - Diwani Maputi | -Mjumbe |
| 11. | Mhe. | Bakari C. Mniyopa | - Diwani Malatu | -Mjumbe |
| 12. | Mhe. | Amina Mkanangwamba | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 13. | Mhe. | Sauda R. Rashidi | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 14. | Mhe. | Athumani M. Mniwasa | -Diwani Chiwonga | -Mjumbe |
| 15. | Mhe. | Munga Mohamedi | - Diwani Mchemo | -Mjumbe |
| 16. | Mhe. | Jamali J. Nandonde | - Diwani Chilangala | -Mjumbe |
| 17. | Mhe. | Rashidi B. Songoni | - Diwani Chihangu | -Mjumbe |
| 18. | Mhe. | Fabian J. Mahanyuka | - Diwani Mnyambe | -Mjumbe |
| 19. | Mhe. | Hanafi N. Nahonyo | - Diwani Mtopwa | -Mjumbe |
| 20. | Mhe. | Rashidi H. Lugomba | - Diwani Nakahako | -Mjumbe |
| 21. | Mhe. | Raia R. Nang'oko | - Diwani Mikumbi | -Mjumbe |
| 22. | Mhe. | Yahaya A. Lisinge | - Diwani Nandwahi | -Mjumbe |
| 23. | Mhe. | Rashidi Nambomo | - Diwani Mnyeu | -Mjumbe |
| 24. | Mhe. | Selemani M. Hiyari | - Diwani Mkoma II | -Mjumbe |
| 25. | Mhe. | Maua Makubui | -Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 26. | Mhe. | Zainabu R. Mpita | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 27. | Mhe. | Zakina A. Mduma | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 28. | Mhe. | Arabia H. Mkwatile | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 29. | Mhe. | Simon F. Nachingulu | - Diwani Nambali | -Mjumbe |
| 30. | Mhe. | Hadija M. Likwembe | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 31. | Mhe. | Selemani A. Mtili | - Diwani Mkwedu | -Mjumbe. |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA:**

1. Mhe. Rashidi A. Akbar - Mbunge -KwaTaarifa.

**WATAALAMU WALIYOHUDHURIA.**

1. Ndg. Shakira Ahmadi – Afisa Utumishi (W)
2. Eng. Sylvester A. Balama - Mhandisi Ujenzi (W)
3. Ndg. Innocent Magayane - K/Mweka Hazina (W)
4. Ndg. Benaya Sanane - Mchumi
5. Ndg. Christina Kambuga - Afisa M/Jamii (W)
6. Ndg. Msafiri Ngai - Afisa Ugavi
7. Ndg. Wilson F. Mafumba - Mkaguzi wa Ndani (W)
8. Ndg. Magreth Likonda - Afisa Ardhi,Maliasili na Mazingira (W)
9. Ndg. Kalugendo Majidu - Afisa Elimu Sekondari (W)
10. Ndg. Juma I Malilo - kaimu Mhandisiwa Maji (W)
11. Ndg. Nsajigwa Mwakatika - Kaimu Katibu TSC (W)
12. Ndg. Mahundu Innocent - Afisa Ushirika (W)
13. Ndg. Omary Msuya - Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
14. Ndg. Rogers Muganyizi - Afisa Ardhi (W)
15. Dr. Judith Ringia - Mganga Mkuu (W)
16. Ndg. Benjamini Macha - Kaimu Afisa Usafirishaji
17. Ndg.Yusufu S.Mshamu - Afisa Tarafa Chilangala.
18. Ndg.Jamila Nalinga - Mtendaji Kata Muungano.
19. Ndg.Boke Mwita - Mtendaji Kata M/Mpelepele.
20. Ndg.Frank Ntilla - K/Mratibu wa UKIMWI
21. Ndg.Shada Nankoko - K/Afisa Utamaduni
22. Ndg.Samuli A. Ali - K/Mtendaji Kata Mkwedu
23. Ndg.Mussa Mohamedi - K/Mtendaji Kata Mpwapwa
24. Ndg.Selemani Aibu - Mtendaji Kata Mtunguru
25. Ndg.Musa E. Musoma - K/Afisa Elimu Sekondari
26. Ndg.Batuli Nahoda - Mtendaji Kata Mnyambe
27. Ndg.Victoria Lusana - Afisa Tarafa Kitangari
28. Ndg.Agness Mnipalika - Mtendaji Kata Mchemo
29. Ndg.Rukia M. Abeid - Mtendaji Kata Chitekete
30. Ndg.Omari Lyopoto - Mtendaji Kata Chiwonga
31. Ndg.Saidi Ussi - Mtendaji Kata Mnyeu
32. Ndg.Hamisi J. Saidi - K/Mtendaji Kata Mikumbi
33. Ndg. Alford Mpanda - Afisa Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika (W)
34. Ndg.Faraji K. Chiponda - Mtendaji Kata Nambali

35. Ndg.Haulii H. Hamisi - Mtendaji Kata Malatu
36. Ndg.Salumu Hassani - Mtendaji Kata Mtopwa
37. Ndg.Amina Mbelenje - K/Mtendaji Kata Maputi
38. Ndg.Selemani Chivambo -K/Mtendaji Kata Nakahako
39. Ndg. Machacha Abdala - Mtendaji Kata Kitangari
40. Ndg. Halfani Halfani - Mtendaji Kata Nandwahi
41. Ndg.Salumu Gheo - Mtendaji Kata Makukwe.
42. Ndg.Emmanuel Msuya - Afisa Utumishi

**WAGENI WAALIKWA WALIOHUDHURIA**

1. Ndg. Edward L. Mukama - Mkuu wa TAKUKURU (W)
2. SSP Jonam Sande - Mkuu wa GEREZA
3. Ndg. Edwin R. Kazengo - Meneja Makonde
4. Ndg. Omary Hisha - Kaim Mkuu wa Polisi (W)
5. Ndg. Celestin Simon Msinje - Mshauri wa Mgambo (W)
6. Ndg. Shabani N. Fungameza - Kaim Afisa Uhamiaji (W)
7. Ndg. Adam Juma - Mwandishi wa Habari TBC
8. Ndg. Mary Santiwa - Mwandishi Gazeti la Mwananchi
9. Ndg. Mohamed Mwaya - Mwandishi wa Habari AZAM TV

**SEKRETARIETI**

1. Ndg. Rashidi Mabaya - Mwandishi wa vikao.

**MUHTASARI NA. 17/2016/2017: KUFUNGUA MKUTANO:**

Mwenyekiti aliwasalimu Wajumbe na wageni waalikwa na kuwataka kushiriki kikamilifu katika Mkutano wa Baraza la Madiwani kwa robo ya tatu 2016/2017. Alifungua Mkutano saa 4:30 asubuhi.

**MUHTASARI NA. 18/2016/2017: KUTHIBITISHA AGENDA:**

Wajumbe walithibitisha agenda zilizowasilishwa na kuridhia zijadiliwe katika kikao.

**MUHTASARI NA. 19/2016/2017: KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 31/01/2017**

Wajumbe walipitia Muhtasari kwa umakini ukurasa hadi ukurasa na kufanya marekebisho yafuatayo:

**Uk. 5**

Neno Vipaombele isomeke Vipaumbele.

Baada ya Marekebisho hayo wajumbe waliupokea muhtasari na kuridhia uwekwe saini ili uwe kumbukumbu sahihi ya kikao.

**MUHTASARI NA. 20/2016/2017 - YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 31/01/2017:**

Muhtasari Na 14/2016/2017 Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo robo ya pili 2016/2017.

***Agizo***

Mwenyekiti wa Halmashauri,Mkurugenzi Mtendaji na Mhandisi wa Maji waende kuongea na wananchi wa Nambali kuhusu Mabomba ya Maji

***Utekelezaji***

Agizo limezingatiwa, Taarifa rasmi itatolewa siku ya Mkutano wa Baraza.

Wajumbe waliridhia utekelezaji huo na hakukuwa na majadiliano.

**MUHTASARI NA. 21/2016/2017 KUPITIA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA TATU 2016/2017:**

Kaimu Afisa Mipango (W) aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo robo ya tatu kwa mwaka 2016/2017 Kwa kusema kuwa katika mwaka **2016/2017** Halmashauri inaendelea kutekeleza miradi ya maendeleo yenye jumla ya thamani ya shilingi **11,899,130,924/=** Kati ya hizo shilingi **934,707,803/=** ni fedha za bakaa ya mwaka **2015/2016** na shilingi **10,886,423,121/=** ni fedha iliyoidhinishwa katika bajeti ya mwaka **2016/2017.**

Hadi kufikia 31 Machi, 2017 Halmashauri imepokea jumla ya shilingi **5,766,406,283** kati ya hizo shilingi **5,673,242,506/=** ni zile zilizopo katika bajeti iliyoidhinishwa na Tshs **93,163,777/=** ni fedha zilizopokelewa nje ya bajeti, ikiwa Tshs **12,000,000/=**ni fedha kutoka ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa ajili ya upanuzi wa miundombinu ya Sekondari Mnyambe na Tshs **81,163,777/=** kwa ajili ya sekta ya Elimu (P4R)

Mpaka kufikia Tarehe 31 Machi, 2017 Halmashauri imeshatumia jumla ya Shilingi **5,866,481,040/=** kutoka kwenye mapato ya ndani na bakaa ya mwaka 2015/2016 katika kutekeleza miradi mbalimbali.

Aidha hadi mwishoni wa robo ya tatu ya mwaka **2016/2017** Jumla ya fedha zote zilizopokelewa kutekeleza shughuli za miradi ya maendeleo ni asilimia **52** ya bajeti iliyoidhinishwa.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili kama ifuatavyo:-

Uk 3

Mjumbe alishauri kuwa katika utekelezaji wa Miradi vipolo kuanishwe maeneo husika.

Mjumbe alisema kuwa Shule ya Sekondari Chihangu kuna tatizo la Meza na Viti.

Mkurugenzi Mtendaji alijibu kuwa matengenezo ya viti na meza yanaendelea yakikamilika shule zote zitapatiwa viti na meza.

Mjumbe alihoji ni lini vifaa vya ujenzi vilivyonunuliwa kwa fedha ya mfuko wa Jimbo vitapelekwa sehemu husika?

Afisa Mipango alijibu kuwa kwa sasa hatua iliyofikia ni hatua za mwisho za manunuzi hivyo ikikamilika usambazaji utaanza.

Mjumbe alihoji ni lini mradi wa maji Makukwe utakamilika?

Mkurugenzi Mtendaji alijibu kuwa changamoto iliyopo hadi sasa ni kipande cha Machenje – Mitema mabomba yaliyoletwa ni machache hivyo mabomba yakiletwa na kuwekwa mradi wa Makukwe utaanza kutoa maji.

Mjumbe alishauri kuwa suala la Kipande cha Mtongwele – Mitema ni bora liombewe Wizarani ili kuweza kutatua tatizo lililopo.

Mjumbe alisema kuwa katika shule ya Msingi Muungano kuna nyumba ambayo imetelekezwa zaidi ya miaka nane (8) na hakuna kinachoendelea, je Halmashauri ina mpango gani wakumalizia nyumba hiyo?

Afisa Mipango alijibu kuwa nyumba hiyo itaingizwa kwenye mpango wa kumalizia miradi vipolo.

Baraza liliagiza kwa Afisa Elimu Msingi aende kufuatilia na kujua changamoto zilizojitokeza kwenye nyumba hiyo.

**TASAF**

Mjumbe alihoji kwa nini miradi ya ajira ya muda kwa kaya masikini wataalamu hawafiki kwenye kusimamia miradi hiyo?

Mratibu wa TASAF alijibu kuwa wataalamu wanafuatilia na kusimamia miradi hiyo.

Mjumbe alishauri kuwa katika mradi wa barabara wa kaya masikini Kijiji cha Chihangu wataalamu waende wakashauri jinsi ya kutengeneza barabara,kwani barabara iliyotengenezwa upana wake ni mdogo.

Mjumbe alishauri kuwa pindi miradi inapoibuliwa kwa kaya masikini ni bora Waheshimiwa Madiwani wajulishwe.

## MUHTASARI NA. 22/2016/2017 KUPITIA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO YA KATA :

Mwenyekiti aliwakaribisha Waheshimiwa Madiwani kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa Kata zao.

### KATA YA CHITEKETE

Mwenyekiti wa kamati ya maendeleo ya Kata ya Chitekete aliwasilisha taarifa ya maendeleo ya kata yake.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo:

Mjumbe alihoji je kuna mpango gani wakuhamasisha wananchi kujiunga na CHF?

Mwenyekiti wa kamati ya maendeleo kata ya Chitekete alijibu kuwa uhamasishaji utafanyika kwa kupitia Mikutano ambayo imeshapangwa kufanyika.

### KATA YA CHIHANGU

Mwenyekiti wa kamati ya maendeleo ya Kata ya Chihangu aliwasilisha taarifa ya kata yake.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo:

Mjumbe aliuliza kuwa ni njia zipi zinatumika kuzuia Mimba kwa wanafunzi katika shule ya Sekondari Chihangu?

Mwenyekiti wa kamati ya maendeleo ya Kata ya Chihangu alijibu kuwa njia moja wapo ni kuongea na wazazi kuhusu madhara ya ujauzito kwa watoto na pia watoto wanapewa elimu ya kutosha kuhusu madhara ya mimba.

### KATA YA MUUNGANO

Mwenyekiti wa kamati ya maendeleo ya Kata ya Muungano aliwasilisha taarifa ya kata yake.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo:

Mjumbe alihoji ni jitihada zipi zimefanyika ili kuweza kupata darasa la awali katika shule ya Muungano?

Mwenyekiti wa kamati ya Maendeleo kata ya Muungano alijibu kuwa jitihada zimefanyika na hadi sasa boma limeshajengwa.

**KATA YA MNYEU**

Mwenyekiti wa kamati ya maendeleo ya Kata ya Mnyeu aliwasilisha taarifa ya kata yake.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na hakukua na majadiliano.

**MUHTASARI NA. 23/2016/2017: KUFUNGA MKUTANO:**

Mwenyekiti wa Mkutano aliwashukuru wajumbe na wageni waalikwa katika mkutano wa Baraza la Madiwani kwa robo ya tatu 2016/2017 kwa mahudhurio yao na ushiriki mzuri katika kuhoji na kujadili agenda zote. Alifunga mkutano saa 9 : 20 alaasiri.

**UMETHIBITISHWA:**

| **Mwenyekiti** | **Katibu** |
|---|---|
| Jina: CHIWANGA R. NDEMBO | Jina: MUSA R. CHIMAE |
| Saini: [signature] | Saini: [signature] |

Tarehe: 30.07.2017